**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 21 Februari, 2025.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2024/2025.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

130. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

(a) Ni taasisi ngapi mpaka sasa zimeshasaini hati za mashirikiano ya utekelezaji wa pamoja wa majukumu yao baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

(b) Ni taasisi ngapi na zipi ambazo ziko njiani kukamilisha zoezi hilo.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

172. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna kila aina ya ushahidi na matendo ya kuthibitisha kwamba kumekuwa na biashara za ukahaba ulio wazi katika kiota cha Gymkana kilichopo Unguja hasa nyakati za usiku.

(a) Je, ni sheria ipi inayoruhusu biashara kama hiyo kuendelea katika kiota hicho ndani ya Zanzibar.

(b) Je, ni utaratibu upi hutumika kupata kibali kwa biashara kama inayofanyika Gymkana.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

37. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Wizara kupitia sekta husika ya utalii inatumia utaratibu gani wa kutoa tuzo kwa wadau na taasisi zilizofanya vyema katika muktadha mzima wa kukuza, kuutangaza na kuudumisha utalii wa ndani na nje ya nchi yetu.

39. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ni kwa kiasi gani Wizara yako inatumia fursa ya matangazo kwenye vyombo vya habari vya kimataifa, majukwaa ya kidijitali, tovuti za utalii na blogu za usafiri katika kuutangaza, kuukuza na kuudumisha utalii wetu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

158. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Kwa kiasi gani teknolojia inasaidia kuendelea kukuwa kwa lugha yetu adhimu ya Kiswahili duniani.

(b) Tathmini iko vipi juu ya ongezeko la vyuo vikuu mbalimbali duniani kuamua kufundisha lugha ya Kiswahili.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

88. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na muamko mkubwa wa wakulima wa mboga mboga kulima kilimo cha biashara (agri-business), ingawa wanakosa elimu ya kilimo hicho na usimamizi thabiti wa kuwalinda zidi ya madalali wanaowakosesha kupata thamani halisi ya biashara hiyo.

(a) Je, ni upi mpango jumuishi wa Wizara yako na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda katika kuchukua hatua za kuimarisha kilimo cha biashara cha mboga mboga chenye tija.

(b) Ni lini Serikali itaanzisha mpango wa pamoja wa kuwahakikishia wakulima wetu wa mboga mboga wanayafikia masoko ya utalii na miradi mikubwa inayokuwa kwa kasi hapa nchini.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

154. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa mfumo wa elimu wa sasa unamuandaa mhitimu kuwa na uwezo wa kujiajiri mwenyewe.

(a) Je, Wizara haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuvisaidia vyuo vya amali kikiwemo Chuo cha Wajasiriamali Mwanakwerekwe, ili kuwawezesha

vijana kufikia malengo ya kujiajiri wenyewe.

(b) Ni mambo gani hasa yanayopelekea changamoto ya uhaba wa ajira nchini.

(c) Serikali inalichukulia vipi wazo la kuwapatia zabuni (tender) za kazi kwa kuvipa kipaumbele vyuo vyetu mbali mbali vya amali kikiwemo Chuo cha Wajasiriamali cha Mwanakwerekwe ili kuchochea upatikanaji wa ajira kwa vyuo kama hivi.

175. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni jambo la kupongezwa kwa Serikali kutoa maelekezo kwa skuli binafsi kutowazuia wanafunzi kuendelea na masomo kwa sababu tu kuna madeni ya wazee/walezi ya kutowalipia watoto wao ada za masomo pamoja na gharama nyengine. Hata hivyo, suala hili halijapata mbadala wake hasa kwa wazee/walezi ambao ni wadaiwa sugu.

(a) Je, Serikali imetoa maelezo gani juu ya ulipaji wa ada unaocheleweshwa unaoathiri uendeshaji wa skuli binafsi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia skuli binafsi zinazokwama kuendesha shughuli zao kwa sababu ya malimbikizo makubwa ya madeni ya ada kutoka kwa wazee/wazazi.

(c) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wanafunzi wa vyuo hawazuiwi kuendelea na masomo/mitihani pale ambapo HESLB au ZHESLB imechelewa kulipa ada za wanafunzi hao vyuoni.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

69. MHESHIMIWA AZZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Uchunguzi wa maradhi yasiyo ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na kansa, unaonekana kuchukuwa muda mrefu bila ya kubainika tatizo halisi.

(a) Nini hasa sababu inayopelekea hali hii.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na magonjwa

haya.

85. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuwepo kwa milipuko ya magonjwa ya kuharisha na kutapika hasa katika kipindi cha mvua, kunatokana na kuzagaa kwa uchafu na kuwepo kwa elimu duni ya afya katika jamii zetu.

Je, ni upi mkakati thabiti wa Wizara yako katika kukiimarisha kitengo cha elimu ya afya kwa wananchi ili kuimarisha utoaji wa elimu endelevu na sio tu pale milipuko inapojitokeza.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

12. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na uchukuzi:

Baadhi ya vijiji katika jimbo la Mtambwe, kama vile Kidundo, Chanjaani na Kiapaka vimekumbwa na tatizo la upatikanaji hafifu wa mawasiliano kutokana na matatizo ya mtandao (network) kuwa dhaifu, hali inayosababisha ukosefu wa mawasiliano. Tatizo hili linaathiri harakati za maendeleo katika vijiji hivi.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani katika kuwasaidia wananchi hawa.

(b) Je, ni ipi tathmini ya kupatikana mawasiliano katika maeneo ya visiwa kwa upande wa Pemba.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ya mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**21 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**